



MATOKEO MAKUBWA SASA (BRN) KATIKA SEKTA YA ELIMU NCHINI, Mpwapwa Tuko Wapi Sasa?

Muhtasari Na. 1

April, 2014

Tanzania, katika kipindi cha zaidi ya miongo miwili sasa imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kimkakati na kisera kuboresha mfumo wa utoaji elimu nchini. Katika kipindi hiki, Tanzania imeshuhudia sera, mikakati na programu mbalimbali zinazolenga kuboresha mfumo wa elimu nchini hususani kuinua kiwango cha elimu ya msingi na sekondari. Pamoja na uwepo wa jitihada hizi, sekta ya elimu nchini bado inakabiriwa na changamoto nyingi kufikia lengo la elimu bora kwa Watanzania.

Takribani miaka miwili sasa, tangu Tanzania izindue mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) nchini, sekta ya elimu ni miongoni mwa sekta zilizo pewa kipaumbele cha kwanza na serikali. Wajibika ikiwa ni miongoni mwa wadau wa sekta hii imeamua kuanza kutathimini ufanisi wa mpango huu kwa shule za msingi Wilayani Mpwapwa.



Kuhusu Programu: Tanzania imeshuhudia jitihada mbalimbali za kuimarisha ubora wa elimu nchini, ikihusisha programu ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ambayo inalengo la kuhakikisha jitihada za kuimarisha elimu zinaleta matokeo ya haraka kwa ufanisi. Wakati jitihada hizi zikipewa nafasi kubwa na serikali, ni dhahiri kuwa bila dhamira ya dhati kisiasa, kiuchumi na kitamaduni; Tanzania, itachukua muda mrefu kufikia malengo haya. Hivyo basi, Wajibika kwa kutambua hilo kupitia mpango mkakati wake wa miaka mitano (2014/2019) imeanza kuunga mkono jitihada hizi kwa kuhakikisha kuwa dhamira ya serikali kuleta matokeo ya haraka kwenye sekta ya elimu inafikiwa kwa kuimarisha mifumo ya utoaji wa elimu bora Wilavani Mwapwa

Utangulizi

Kusudi la utafiti huu ilikuwa ni Kutathmini ubora wa elimu kwa ujumla kuanzia ngazi ya uongozi mpaka kwenye matokeo ya shule husika katika wilaya ya Mpwapwa mkoa wa Dodoma katika shule za msingi. Ilikusudiwa kuwa lengo hili la jumla lingepimwa kwa kutumia malengo mahususi yafuatayo, Kubaini uwiano wa waalimu na wanafunzi katika shule, Kubaini hali ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vinaendana na idadi ya wanafunzi, Kubaini uhusiano kati ya ufaulu wa wanafunzi na viwango vya elimu kwa walimu na pia Kubaini umuhimu wa mafunzo kazini unavyochangia ubora wa elimu.

Kwa muda mrefu inaonekana kuwa hakukuwa na utafiti uliofanyika katika wilaya ya Mpwapwa hususani kubaini ubora wa elimu Wilayani. Swala hili ndilo lililosukuma asasi ya Wajibika kuamua kufanya utafiti huu kwa awamu ya kwanza kwa kuamini kuwa utawasaidia wadau wote wanaohusika na maswala ya elimu nchini. Nimatarajio yetu kuwa utafiti huu utasaidia kujua uhalisia wa tatizo jambo ambalo litasaidia hatuwa stahiki kuchukuliwa na hatimae kuinua ubora wa elimu na hivyo kufikia malengo ya seriakali ya kupata Matokea makubwa sasa (BRN) pamoja kufikia malengo ya Millenia (MDGs)

Utafiti huu ulifanyika kwa uwakilishi wa maeneo ya mjini na maeneo ya Vijijini lengo likiwa ni kupata uhalisia wa ubora wa elimu katika maeneo yote. Mtindo huu wa uwakilishi(sampuli) unakubalika sana na wataalam wa tafiti mbalimbali ulimwenguni. Kwa mfano (Kothari, 2004) alisema sio rahisi kuwafikia watu wote washiriki katiaka utafiti, hivyo kutumia uwakilishi ni swala lisiloepukika katika utafiti. Lengo la kuchagua maeneo ya mjini ilikuwa ni kupata taarifa ambazo zingeonesha hari ya ubora wa elimu katika maeneo hayo, pia shule za vijijini zilichaguliwa ili kusaidia kupata ulinganisho kati ya maeneo ya mjini na vijijini. Tukiamini kuwa taarifa hizo zitawasaidia wasimamizi wa elimu kutoa mgawanyo sawa wa rasilimali za kutolea elimu katika maeneo yote, hivyo kuleta usawa wa elimu na hatimaye kufikia lengo la serikali la kutoa elimu kwa usawa na lengo la Umoja wa Mataifa (1948) la elimu sawa kwa wote. (EFA=Equal Education for All).

Shule za maeneo ya mjini zilizoshiriki katika utafiti huu ni Mtejeta, Chazugwa, Mpwapwa, Vinghawe, Igovu, Kikombo na Ilolo. Na kwa upande wa shule za vijijini zilizo shiriki katika utafiti ni Pwaga, Lumuma na Matomondo shule ya msingi. Katika kurasa zinazofuata zinabainisha matokeo ya utafiti pamoja na ushauri uliotokana na matokeo ya utafiti huu.

Matokeo ya utafiti

Katika kipindi chote cha utafiti asasi ikitumia wataalamu wake makini ilikuwa inafuatilia na kukusanya taarifa kwa umakini mkubwa, baada ya taarifa kukusanywa zilichambuliwa na kupembulia kwa kutumia njia za kitaaluma na kisayansi na hatimae kupata majibu yafuatayo:-

Uwiano wa Walimu na Wanafunzi Katika Shule

Asasi ya Wajibika ilikusudia kupata taarifa za uwiano wa Walimu na Wanafunzi katika baadhi ya shule za msingi wilayani Mpwapwa, katika kupata majibu ya swala hili watafiti walitumia njia ya dodoso kupata majibu kutoka kwa washiriki.

Jedwali namba 1: Uwiano kati ya Mwalimu na Wanafunzi

Shule	Idadi/wanafunzi	Idadi/walimu	Uwiano	
			Walimu	Wanafunzi
Mtejeta	831	36	1	23
Pwaga	891	18	1	49
Ilolo	653	34	1	19
Igovu	441	22	1	20
Mpwapwa/msingi	628	28	1	22
Kikombo	528	26	1	22
Matomondo	726	22	1	32
Ving'awe	956	35	1	27
Chazugwa	823	35	1	24
Lumuma	261	11	1	23

Matokeo ya utafiti katika jedwali namba 1 yanaonesha kwamba shule ya msingi Mtejeta ndio yenye walimu wengi ambapo kuna walimu 36 sawa na uwiano wa wanafunzi 23 kwa kila mwalimu 1, shule ya msingi Pwaga ndio imeonekana kuwa na idadi kubwa zaidi ya wanafunzi ambao ni 891 na walimu 18 sawa na uwiano wa wanafunzi 49 kwa kila mwalimu 1, shule ya msingi Ilolo ina wanafunzi 653 na walimu 34 sawa na uwiano wa wanafunzi 19 kwa mwalimu mmoja. Shule ya msingi igovu ina walimu 22 na wanafunzi 441 sawa na uwiano wa wanafunzi 20 kwa kila mwalimu 1, shule ya msingi Mpwapwa ina walimu 28 na wanafunzi 628 sawa na uwiano wa wanafunzi 22 kwa kila mwalimu 1. Shule ya msingi Kikombo ina wanafunzi 528 na ina walimu 26 sawa na uwiano wa wanafunzi 22 kwa kila mwalimu 1, shule ya msingi Ving'awe ina wanafunzi 956 na walimu 35 sawa na wanafunzi 27 kwa kila mwalimu, shule ya msingi Chazungwa ina wanafunzi 823 na walimu 35 sawa na uwiano wa wanafunzi 24 kwa kila mwalimu 1.

Kwa kuzingatia mchanganuo ulioainishwa hapo juu utafiti unaonesha kuwa wastani wa Uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi kwa shule zote ni wanafunzi 35 kwa kila mwalimu mmoja. Kwa kuzingatia Uwiano huu utafiti unaonesha ikama inaridhisha na inaendana na sera ya elimu ya mwaka 1995 ambayo inaelekeza kwamba ikama kwa shule za msingi itakuwa wanafunzi 45 kwa kila mwalimu mmoja¹. Kwa hiyo mgawanyo wa walimu katika shule hizi zilizohusika katika utafiti unaendana na mahitaji ya sera ya elimu na mafunzo ya ufundi ya mwaka 1995.

¹ Sera ya Elimu 1995

Pamoja na shule hizi zilizohusika katika utafiti huu kuwa na ikama inayo takiwa hata hivyo katika shule ya msingi Pwaga, imeonekana kuwa na Idadi ya wanafunzi wengi zaidi ambayo haiendani na ikama ya wanafunzi 45 kama sera inavyoelekeza, badala yake ikama inaonesha ni wanafunzi 49 kwa kila mwalimu mmoja. Hivyo kwa kuzingatia utafiti huu tunashauri walimu waongezwe katika shule hii ili kuendana na ikama inayotakiwa, iwapo hali hii itaendelea kuwa hivi ubora wa elimu katika shule hii utashuka.

Katika shule za msingi Tanzania kila mwalimu anatakiwa awe na vipindi 28 kwa wiki na kila mtoto kwa kuanzia darasa la tatu anatakiwa apate vipindi 40 kwa wiki. Kwa kuzingatia uwiano uliobainika hapo juu shule karibu zote walimu wanatoshereza kukidhi mgawanyo huo. Hivyo asasi inaamini kama walimu watawezesha kupewa mazingira bora ya kufanyia kazi adhima ya elimu bora itafikiwa katika shule hizi.

Kwa kuzingatia uwiano uliobainika hapo juu, shule karibu zote walimu wanatoshereza kukidhi mgawanyo huo

Uwepo wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia Katika Shule

Utafiti ulionesha kuwa katika shule zote zilizoshiriki katika utafiti, kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Washiriki waliojibu dodoso la utafiti walitoa majibu ambayo yalikuwa yanathibitisha kuwa shule zinahaba mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Jedwari namba 2 linabainisha majibu ya washiriki:-

Jedwari namba 2: Hali ya Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kujifunzia Mashuleni

Washiriki	Ndiyo	Hapana	% Ndiyo	% Hapana	%Jumla
10	10	0	100	0	100

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba jumla ya washiriki 10 ambao waliwakilisha shule 10 za msingi, majibu yao katika jedwali yanabainisha kuwa shule zinakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Asilimia 100 ya washiriki ambao wote walikuwa walimu wakuu wa shule wanakubali kuwa kuna tatizo la vifaa mashuleni. Hii inamaanisha kuwa vifaa kama vitabu vya kiada na ziada, madawati, vyumba vya madarasa, mbao za kuandikwa, meza na viti vya walimu, ofisi za walimu na maktaba kwa ajili ya wanafunzi na walimu kujisomea havitoshelezi mahitaji.

Suala la vifaa vya kujifunzia na kujifunzia limebainika kuwa ni suala nyeti na mhimu katika kufanikisha mafunzo kwa mwanafunzi, tafiti mbalimbali zilizofanyika zinaonesha kuwa “vifaa vinavyotumika kutolea elimu vinamsaidia mwalimu na mwanafunzi katika kutoa na kupata elimu²” Hivyo majibu ya utafiti huu katika kipengele cha vifaa vya kutolea elimu yametoa sura halisi ya hali ya upatikanaji wa vifaa katika shule za msingi wilayani Mpwapwa kuwa ni duni inayohitaji uwekezaji zaidi katika eneo hilo la vifaa.

Majibu kutoka kwa washiriki pia yanaonesha kuwa hakuna tofauti ya hali ya upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika maeneo yote ndani ya wilaya, washiriki wote kutoka katika shule za mjini wametoa majibu yanayoonesha kuwa hakuna vifaa, hali kadhalika majibu ya washiriki kutoka

² Mosha, 2000


katika maeneo ya shule za vijijini nao pia wametoa majibu yanayo fanana na washiliki wa mjini. Kufanana kwa majibu haya kunafanya tafiti hii ijenge hoja na kuamini kuwa hali ya upatikanaji wa vifaa vya kutolea elimu Wilayani ipo chini kiwango ambacho hakiridhishi kufikia malengo ya serikali ya kutoa elimu bora kwa watu wote na lengo la matokeo makubwa sasa.

Majibu ya matokeo ya utafiti huu yamefanana na majibu ya tafiti zilizotangulia kufanywa na watafiti mbalimbali, ambapo katika tafiti zao walibaini kwamba “ukitaka kujua kiwango cha ubora wa elimu utaangalia uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi, ghalama za kumsomesha mwanafunzi, ubora wa walimu wanaofundisha na vifaa vilivyopo shuleni³”. Tafiti hizi pamoja na utafiti huu zinathibitisha kwamba elimu bora itapatikana iwapo tu kutakuwa na mazingira ya kuridhisha ya vifaa vya kutolea elimu katika mashule.

Uhusiano Kati ya Ufaulu wa Wanafunzi na Viwango vya Elimu kwa Walimu

Katika utafiti huu asasi yetu ilitaka kupata na kujua iwapo kuna uhusiano wowote kati ya kiwango cha elimu cha mwalimu anaefundisha na ufaulu wa mwanafunzi katika matokeo yake ya mwisho ya mtihani. Ili kupima lengo hili washiriki wa utafiti walipewa dodoso lililohitaji wataje viwango vya elimu za walimu kwa shule zao na hali ya ufaulu wa shule kwa kipindi cha miaka mitatu (2010 - 2012), ili taarifa zitakazo patikana zitumike kufanyia ulinganisho na matokeo ya wanafuzi na hatimae kupata majibu ya lengo hili. Baada ya taarifa kupembuliwa kwa umakinifu jedwali namba 3 na 4 yanaonesha majibu ya washiriki wa utafiti:-

Jedwali Namba 3 la Matokeo ya Mitihani 2010-2012



³ Dearden, Ferry & Meghir 2002, Ishikawa and Ryan 2002, Mosha 2000 na Wilson 2001

Jedwali namba 4 Viwango vya elimu kwa walimu

	Daraja B/C	Daraja III A	Diploma	Shahada	S/Uzamili
Mtejeta	-	24	9	1	2
Lumuma	-	11	-	-	-
Ilolo	-	33	-	1	-
Igovu	-	21	1	-	-
Pwaga	2	15	1	-	-
M/msingi	-	27	1	-	-
Vinghawe	-	33	1	1	-
Chazugwa	-	31	3	2	-
Matomondo	-	22	-	-	-
Kikombo	-	23	2	1	-

Matekeo ya utafiti katika majedwali yote 2, yanabainisha kuwa kuna uhusiano mkubwa sana kati ya ufaulu wa wanafunzi na viwango vya elimu vya walimu. Katika shule zote kumi ambazo zilihusika katika utafiti huu, imebainika kwamba walimu wote wana sifa zilizowekwa kwa mtu kuwa mwalimu wa shule ya msingi. Majibu haya yameendana na maelekezo ya sera ya taifa ya elimu ya mwaka 1995, ambayo emelekekeza kwamba sifa ya mwalimu wa shule ya msingi ni kuanzia kiwango cha ngazi ya astashahada ya ualimu (grade A).

Hata hivyo kwa baadhi ya shule utafiti ulionesha kuwa kuna walimu ambao wana viwango vya elimu zaidi ya astashahada. Kwa mfano katika shule ya msingi Mtejeta utafiti ulionesha kuwa walimu 9 wana diploma, 1 shahada na 2 wana shahada za uzamili. Utafiti ulionesha kuwa katika shule hii wanafunzi wanakuwa na alama kubwa zaidi za ufaulu, jambo ambalo huwa linadhihirishwa na idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuingia katika shule za kitaifa, katika upembuzi wa matokeo ya mtihani wa darasa la saba, ilibainika kuwa jumla ya wastani wa alama za ufauzi katika shule ya msingi Mtejeta ni wa juu zaidi ukilinganisha na shule nyingine zilizoshiriki katika utafiti, tofauti hizi zinatokana na ukweli uliojibainisha kwenye utafiti huu, kwamba shule ya msingi Mtejeta inawalimu wenye viwango vya juu zaidi kielimu ukilinganisha na shule nyingine kama nilivyotaja awali. Ukweli huu unadhihirisha kuwa kadri shule inavyokuwa na walimu wenye elimu za juu ndivyo ubora wa elimu unavyozidi kuwa bora zaidi. Majibu ya utafiti huu unaendana na sera ya elimu ya nchi ya China inayotumika hivi sasa inayosema kwamba “ili mtu awe mwalimu katika shule za msingi za China ni lazima awe na elimu ya kuanzia shahada ya kwanza⁴”

Tafiti zinabainisha kwamba mwalimu anavyokuwa na elimu ya juu zaidi, ndivyo anavyokuwa na uwezo zaidi wa kumudu njia za kufundishia na uwezo wa kitaaluma⁵. Pia tafiti zinabainisha kwamba wanafunzi wanakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kupata haki ya elimu bora ambayo ni lengo ambalo serikali imejiwekea na pia ni lengo la mpango mkakati wa mkutano wa elimu wa Dakar na mpango wa maendeleo wa milenia⁶

⁴ Kimaryo, 2011

⁵ UNESCO, 1978

⁶ Dakar Framework for Action on Education for All (EFA) and the World Summit Millennium Development Goals (MDGs)

Kwa hiyo basi, utafiti huu unatupa picha halisi ya namna kiwango cha elimu ya mwalimu anaefundisha kinavyo athiri ubora wa elimu katika nchi. Ni muhimu serikali iwekeze zaidi katika kuwaendeleza walimu kitaaluma ili kuwajengea uwezo zaidi. Pia ni mhimu serikali itekeleze sera ya elimu na mafunzo ya ufundi kwa vitendo kama inavoeleza wazi kwamba kila mtanzania na hasa watoto wapate nafasi ya kupata elimu bora, ikiwa ni moja ya haki za binadamu. Mpango wa PEDP unasisitiza kuwa, kuwaendeleza walimu kitaaluma itakuwa ni moja ya mbinu za kufikia lengo hilo⁷. Sanera (1998) alisema walimu wanahitaji mafunzo ya kuendelezwa kitaaluma wakiwa kazini na wanapokuwa masomoni, ili kuwaweka waende sambamba na mabadiliko ya sasa ya sayansi.

Kubaini Umuhimu wa Mafunzo Kazini Unavyochangia Ubora wa Elimu

Katika kupima umuhimu wa mafunzo kwa walimu, Asasi iliwauliza maswali ya ana kwa ana (interview) walimu wakuu kumi, maswali yalikuwa ya wazi yakiwataka watowe maoni yao, iwapo mafunzo ya kazini kwa walimu yana mchango wowote katika kuboresha elimu.

Washiriki wote kumi ambao walikuwa wanawakilisha shule kumi za msingi, walieleza kwa kina jinsi mafunzo ya kazini yanavyotowa mchango katika kuboresha elimu. Walisema kumekuwa na uhaba mkubwa wa mafunzo kazini kwa walimu wakuu na hata walimu wakawaida wanaofundisha mashuleni. Kwa mfano mshiliki mmoja kutoka shule X alisema:-

“Tangu nipate nafasi hii ya mwalimu mkuu kwa muda wa miaka miwili sasa, sijawahi kuhudhuria mafunzo yoyote ya kunjengea uwezo wa kiutawala na hata kitaaluma, naongoza shule kwa kutumia uzoefu wangu na ujuzi mdogo nilioupata wakati nasomea kazi ya ualimu”

Majibu ya mwalimu huyu kutoka shule X yanatupa picha ya hali halisi ya utowaji wa mafunzo kazini kwa walimu katika wilaya ya Mpwapwa kuwa ni ndogo. Pia tunapata picha kwamba wakuu wa shule za msingi wanaongoza shule kwa kutumia uzoefu na ujuzi mdogo wanaoupata wanapokuwa vyuoni/shuleni, katika mtaala wa kuwaandaa walimu wa shule za msingi kwenye vyo vya ualimu unaotumika sasa, somo la mafunzo ya uongozi kwa walimu halijatajwa kama somo linalojitegemea bali hujitokeza mara chache ndani ya baadhi ya masomo mengine.

Pia majibu ya mwalimu kutoka shule X, yanaonesha hata mafunzo ya kitaaluma ya kuwajenge uwezo walimu ili wafundishe vizuri zaidi hayatolewi kwa wakuu wa shule na walimu wa kawaida. Walimu wameendelea kufundisha kwa kutumia uwezo wao binafsi na ujuzi walioupata wakati wanasomea kazi ya ualimu, jambo ambalo linaathiri umahiri wao, hasa katika dunia ya sasa ya changamoto za mabadiliko ya tekinorojia mbalimbali katika jamii. Mwalimu mwingine kutoka shule Y alisema:-

“Katika kipindi ambacho nimefundisha cha zaidi ya miaka tisa, sijawahi kuhudhuria mafunzo yoyote ya kuendeleza taaluma yangu, kadri siku zinavyozidi kuongezeka ndivyo ninavyozidi kuwa mbali na taaluma mpya inayojitokeza katika ufundishaji, hata kunapokuwa na mabadiliko ya mtaala sijawahi kupewa mafunzo ya namna ya kutekeleza mabadiliko hayo katika mtaala, kwa mfano baada ya serikali kuanzisha somo la TEHAMA katika mtaala ambalo mimi nalifundisha hatukupata mafunzo yoyote ya kutujengea uwezo wa kulifundisha”

⁷ URT - PEDP, 2001

Majibu haya ya mwalimu kutoka shule Y yanabainisha kuwa walimu hawapati mafunzo yoyote wanapokuwa wameajiriwa, wanaendelea kufundisha kwa taaluma walizozipata wakati wanasomo. Hakuna muendelezo wa kuwajengea uwezo wowote wa ziada. Katika utafiti wake Mosha, 2000 alisema “mafuzo kazini kwa walimu ni dhana mhimu sana ya kupata elimu bora” Aidha, tafiti nyingine zinaeleza kwamba mafunzo kazini hakika huzalisha ujuzi binafsi, utaalamu na na uwezo wa kitasnia ambao huongeza uthamani katika mchakato wa uzalishaji wa matokeo⁸

Ni muhimu mafunzo yatolewe kwa walimu wanapokuwa kazini ili kusaidia kufikia malengo ya kupata matokeo bora. Huwezi ukapata matokeo bora kama walimu hawajaendelezwa kuyafikia matokeo bora, kwa mfano kunapokuwa na mabadiliko ya mtaala ni muhimu wapate mafunzo ya namna ya kutekeleza mtaala mpya. Kutokana na uhaba wa mafunzo kwa walimu na hasa kunapokuwa na mabadiliko ya mitaala, shule nyingi kwa sasa zinakabiliwa na tatizo la ugumu wa kutekeleza mhamo wa luwaza (paradigm shift) ambao ndio mfumo unaopendekezwa kutolea elimu kwani unamjengea uwezo zaidi mwanafunzi katika mambo anayojifunza na uhalisia wake katika maisha ya kawaida.

Mtazamo wa Walimu Kuhusu Malipo ya Mishahara

Walimu waliulizwa watowe maoni yao kuhusiana na Viwango vya mishahara vinavyotolewa na serikali kama vinakidhi malipo kwa mwalimu. Walimu walitoa maoni tofautitofauti, katika maoni yote yaliyotolewa na walimu yalionekana kuto kukidhi malipo ambayo yangestahili kwa mwalimu kulipwa kutokana na umuhimu wa kazi ya ualimu ambayo ni kuelimisha jamii. Jedwari namba 5 linaonesha viwango vya malipo ya walimu:-

Jedwali namba 5: Makadilio ya Mshahara wa Mwalimu kwa Mwezi

Majibu ya wahojiwa	Frequency	Asilimia (%)
100001 – 200000	3	30
200001 – 300000	5	50
400001 – 500001	1	10
600000 – kuendelea	1	10
Jumla	10	100

Jedwari namba 5 linaonesha kwamba 50% ya walimu katika shule zilizoshiriki utatafiti wanalipwa mshahara wa kati ya shilingi 200,001 – 300,000 kwa mwezi. 30% wanalipwa kati ya shilingi 100,001 – 200,000 kwa mwezi. 10% ya washiliki wanalipwa shilingi 400,001 – 500,001 kwa mwezi na 10% wanalipwa kuanzia shilingi 600,000 na kuendelea.

Matokeo haya ya utafiti kama yanavyonekana hapo juu yanabainisha kwamba malipo ya mishahara kwa walimu wa shule ya msingi ni madogo ambayo hayatoshelezi mahitaji yao muhimu. Mwalimu anatakiwa alipwe mshahara unaoendana na hali ya maisha na kumfanya aishi kama mtu aliewekeza katika elimu kwa muda mrefu. Malipo ya Ualimu katika Tanzania ukilinganisha na tasnia nyingine yapo chini, kwa mfano daktari mwenye shahada anaanza kazi huanzia mshahara wa TGHOS D.1 (Tsh. 1,102,000/=), mtafiti wa kilimo na mifugo huanza na TGRS C.1 (Tsh. 1,133,600/=) na hakimu

⁸ Mushashu, 2000 & OECD 2009

anaanza kazi huanzia TJS 3.1 (Tsh. 1,012,000/=) na mwalimu mwenye Shahada (Degree) wa chuo cha ualimu huanza na TGTS E1 (Tsh. 720,000/=)⁹

Kutokana na utofauti huu mkubwa wa mishahara ni wazi kwamba walimu wanavunjwa moyo wa kufanya kazi katika vituo vyao vya kazi. Nidhahiri kwamba mwalimu anapoona analipwa kiasi kidogo na serikali ile ile inayolipa tasnia nyingine, moyo wa kufanya kazi unakuwa chini na hata kupelekea kuingia kwenye migomo ambayo inaathari mbaya kwa wanafunzi.

Mwaka 2000 Moshia, katika utafiti wake alibaini kwamba walimu kuanzia na wa shule za msingi hadi vyuo vikuu hawajapewa motisha katika mishahara yao, kwa hivyo wengi wameathirika kisaikolojia, na uwepo wao katika vyuo na shule ni wa muonekano tu, hii inamaanisha kwamba walimu wengi wamepata matatizo kisaikolojia na hivyo utendaji wao wa kazi ni mdogo sana. Mushashu (2000: 1999) katika kuliielezea suala la ugumu wa mazingira ya kazi ya mwalimu alisema “kutokuwepo kwa nyumba za kutosha za walimu, mishahara mdogo na malipo mdogo ya stahili nyingine vinapelekea kuvunjika kwa moyo wa kazi kwa walimu jambo ambalo linasababisha walimu waache kujihusisha na mahitaji ya wanafunzi”

Utafiti huu na tafiti zilizotajwa hapo juu, zinatoa msisitizo mkubwa wa jinsi malipo mazuri kwa walimu yanavyotoa mchango stahiki katika kupata elimu bora. Hivyo ni muhimu serikali ipitie viwango vya mishahara ya walimu upya ili viboreshwe na hatimae kuendana na sekta nyingine kama si kulingana. Ni muhimu pia serikali kuanza kufikilia kuifanya tasnia ya ualimu moja ya sekta muhimu na inayoheshimika nchini. Kwa mfano, tasnia ya ualimu nchini Marekani ni moja ya tasnia zinazolipwa mishahara mkubwa na kuheshimika sana na jamii¹⁰

⁹ Chanzo URT/UTUMISHI, 2012

¹⁰ Babyegeya, 2006

Ushauri kwa Wizara ya Elimu, TAMISEMI na Halimashauri ya Wilaya ya Mpwapwa

Kutokana na matokeo ya utafiti huu mambo yafuatayo yanashauriwa kuzingatiwa:-

- ❖ Uwiano wa ufaulu kwa wanafunzi kati ya wale wa vijijini na mjini unaonekana kulingana kwa maana ya idadi, ila kwa viwango vya ufaulu kwa maana ya alama za ufaulu wanafunzi wa mjini wameonekana kuwa juu zaidi ya wale wa vijijini. Hii inamaana kwamba ikiwa hakutakuwa na msawazo (standardization) wa viwango vya madaraja uwiano wa ufaulu kwa maana ya idadi (number) bado wanafunzi wa vijijini wanakuwa chini sana.
- ❖ Vigezo vya BRN vya ufaulu kwa wanafunzi viangaliwe upya kwani vinaonesha kupima viwango vya chini vya uelewa (lower level of learning) na kuacha viwango vya juu vya uelewa (high level of learning)
- ❖ Mgawanyo wa walimu katika shule uzingatie idadi ya wanafunzi waliopo shuleni ili ikama iendane na mahitaji halisi katika shule
- ❖ Halimashauri kwa kushirikiana na wadau wengine waongeze vifaa vya kufundishia mashuleni
- ❖ Uandaliwe Mpango mkakati wa Wilaya na utaratibu wa kuwapa mafunzo kazini walimu ili kukuza ufanisi wao wa kazi na kuboresha taaluma zao
- ❖ Halimashauri isaidie kuishauri serikali kuongeza mishahara kwa walimu ili iendane na hali ya maisha ya sasa.
- ❖ Idara kwa kushirikiana na walimu wakuu ibuni mikakati zaidi ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi na ubora wa elimu katika wilaya kwa kutumia rasilimali zilizopo.

- Kimaryo, A. L. (2011) Integrating Environmental Education in Primary School Education in Tanzania: Teachers' Perceptions and Teaching Practices. Abo Akademi University press.
- Kothari, R. C. (2004) *Research methodology: Methods and techniques* (2nd rev. ed.). New Delhi. Age International.
- Mosha, H. J. (2000) Conceptualizing quality of education.
- J.C. J. Galabawa, F. E.Senkoro. & A. F. Lwaitama. *The quality of education in Tanzania: Issues and experience* (pp. 1-20).Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- Mushashu, B. (2000) The issues of quality of public secondary schools: What can be done? What ought to be done?
- Ncube, J. N. (2004). *Managing the quality of education in Zimbabwe: The internal efficiency of rural day schools*. (Doctoral thesis. University of South Africa). Retrieved from www.uir.unisa.ac.za/bitstream/handle/10500/619/thesis.pdf
- United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization, (2005). *Education for All: The quality imperative*. Education for All Global Monitoring Report, Paris: UNESCO.
- United Republic of Tanzania, (1995). *Education and Training Policy*. Dar es Salaam, Tanzania: MoEC
- United Republic of Tanzania, (2001). *Education Sector Development Programme: primary education development plan (2002-2006)*. Dar es Salaam, Tanzania: MoEC.
- United Republic of Tanzania, (2012, Julay). *Waraka wa watumishi wa serikali kuhusu marekebisho ya mishahara ya watumishi wa serikali* (Toleo na. 1). Dar es Salaam. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma/ UTUMISHI.